HALMASHAURI YA WILAYA YA MOROGORO
SHULE YA SEKONDARI MATOMBO

ANUANI: MKUU WA SHULE
Simu: +255 714 907 572
+255 717 774 333
Email: matombosecschool@gmail.com

S.L.P. 749,
MOROGORO.

Tarehe: …….

Unapojibu tafadhali taja:

Kumb Na……

Mwanafunzi: ……..
……
……

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA KIDATO CHA TANO SHULE YA SEKONDARI MATOMBO MWAKA 2022

1.0 Karibu Shuleni Matombo.

Kwa niaba ya kamati ya uchaguzi ninayo furaha kukuarifu rasmi kwamba umechaguliwa kujiunga na shule hii. KIDATO CHA TANO mwaka 2022 kwa mchepuo wa:-

HGL **HKL** **HGK** ☐

"JUHUDI MAARIFA NA VITENDO" Maneno haya ndiyo **KAULI MBIU** au mwongozo wa shule yetu. Kama umeridhia kujiunga na shule hii, huna budi kuitafakari kauli hiyo na kuichukulia kwa uzito unaostahili.

Shule ya Sekondari Matombo ipo Halmashauri wilaya ya Morogoro, Tarafa ya Matombo kata ya Konde,ipo umbali wa kilometa 64 kutoka Manispaa ya Morogoro.

Muhula wa kuanza masomo utaanza MAPEMA JULAI unatakiwa kuripoti shuleni TAREHE ITAKAYOTANGANGAZWA NA MAMLAKA YA URIPOTI WA WANAFUNZI KIDATO CHA TANO 2022.

MUHIMU:- Endapo utachelewa zaidi ya wiki mbili utakuwa umepoteza nafasi hii.

2.0 Usafiri kutoka manispaa ya Morogoro hadi shule ya sekondari Matombo.

Ukifika/ukishuka kituo cha mabasi cha Morogoro kiitwacho **Msamvu**, panda daladala zinazokwenda mjini kwa Tshs.400/=, shuka kituo kiitwacho **Kanisani**, nenda mbele kidogo, katiza upande wa kushoto,fuata barabara inayoenda **Kaloleni** (Magari yaendayo Matombo) umbali ni takribami mita 200. Ukichukua Tax kutoka Msamvu stendi hadi Kaloleni stendi nauli ni Tshs.5000/=, kwa usafiri wa Boda Boda ni Tshs.2000/=.

KALOLENI: Ukipanda magari ya Morogoro – Matombo yaendayo **Mtamba** shuka **Msalabani** nauli ni Tshs.6000/= chukua Bodaboda kwa Tsh.1000/= hadi Matombo Sekondari.

KALOLENI: Ukipanda magari ya Morogoro- Matombo yaendayo **Tawa** shuka **Matombo ndani stand** ulizia mahali shule ilipo ni takribani mita 300.

AU

Ukishuka **Msamvu** kituo cha mabasi yaendayo mikoani ulizia kituo cha mabasi yaendayo **Kisaki** kilichopo hapo Msamvu. Nauli ni Tshs.6000/= utashuka **Msalabani** na kuchukua Bodaboda hadi Matombo Sekondari kwa Tshs.1000/=.

3.0 Mambo muhimu ya kuzingatia:-

3.1 Sare ya shule:-

a) Sare ya darasani:-

Sketi mbili rangi ya bluu iliyokolea (Dark blue) inapatikana shuleni – kwa malipo.

Mashati mawili meupe aina ya tomato, mikono mifupi kwa wakristo na mikono mirefu kwa waislamu, yenye "collar" na mfuko kwa kila shati **(Inapatikana shuleni).**

Viatu vyeusi vya kufunga kwa kamba, yenye visigino vifupi (muundo kama viatu vya kiume). **(Aje navyo).**

Soksi nyeupe jozi mbili (02) zisizo na urembo au alama yoyote ya rangi **(Aje nazo).**

Sweta moja rangi ya bluu iliyokolea (Dark bule) **(inapatikana shuleni)** – kwa malipo.

Sare ya kazi :- Sketi rangi ya bluu iliyokolea (Draft ndogo) mshono wa rinda box na T-shirt mbili rangi ya bluu zenye nembo ya shule (vinapatikana shuleni) kwa malipo. **Watakaovaa hijab (zinapatikana shuleni)**

Sare za michezo:- Raba nyeusi, Track suit za michezo zikiwa na nembo ya shule na **UTAMBULISHO** wa mwanafunzi **(zinapatikana shuleni)** kwa malipo. Wakati wa michezo kila mwanafunzi atalazimika kuvaa sare ya michezo hivyo ***wasiliana na uongozi kwa maelekezo zaidi.***

Wanafunzi watavaa sare ya darasani wakati wa vipindi na sare ya kazi baada ya muda wa vipindi. Mwanafunzi aje na sare ya shule **alikokuwa anasoma.** Sare hiyo itatumika kwa muda wakati sare ya shule inashonwa. Nguo za nyumbani **HAZIRUHUSIWI KABISA** hivyo **asije nazo.**

MUHIMU:-

Ili kuleta ulinganifu sawa sare zifuatazo zinapatikana hapa shuleni kwa gharama zifuatazo:-

Sketi mbili (2)
T- shirt mbili(2) za blue zenye nembo
Sweta moja (01) rangi ya dark bluu
Nembo mbili (02) kwa ajili ya mashati mawili (02)
Mashati mawili (2)
Hijabu mbili (2)
Sketi mbili za kazi
Sare ya michezo yenye utambulisho na nembo ya shule.

NB: SARE HIZI ZINAPATIKANA ZOTE SHULENI WASILIANA NA MKUU WA SHULE KWA SIMU

3.2Michango mingine ya shule;-

(i) Michango mingine ni:-

a) Kitambulisho cha mwanafunzi	-	shillingi	5,000/=
b) Ukarabati	-	shilingi	10,000=
c) Taaluma kwa mwaka	-	shilingi	20,000/=
d) Gharama ya picha "passport size"	-	shilling	3,000/=
e) Matroni kwa mwaka	-	shilingi	30,000/=
f) Mpishi kwa mwaka	-	shilingi	20,000/=
g) Mlinzi	-	shilingi	30,000/=
h) Ada/Karo	-	shilingi	70,000/=

Jumla – TSH 188,000/=

Vifaa vya taaluma

-Ream mbili (02) **kwa kila mhula,** moja (01) ya "photocopy" na moja ya (01) ya mistari (rulled). Pia aje na File moja kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu zake. (NI LAZIMA)

Vifaa vya usafi:

Toilet/scrubing brush (01), Softbroom (fagio laini) (01), hard broom (fagio la brashi ngumu 01), Rubber squeezer (fagio la kusukumia maji 01), Reki (01), jembe jipya na mpini wake (01), Dawa ya kusafishia vyoo lita moja (kwa muhula), slasher (fyekeo (01), fagio la chelewa na zoleo la uchafu kwa ajili ya kufanya usafi eneo lake.

Ndoo mbili kubwa (02).

3.3. VYETI NA RESULT SLIPS

-Leta result slip ya kidato cha nne.

- Leta nakala ya cheti cha kuzaliwa.

3.4 MUHTASARI WA GHARAMA ZINAZOHITAJIKA:-

1) Ada/Karo ya shule kwa mwaka	-	shilingi 70,000/=
2) Gharama nyingine (Michango)	-	shilingi 118,000/=
Jumla		**Ths.188000/=**

MUHIMU:- Ulipaji wa ada na michango yote ufanyike tawi lolote la Benki ya NMB. Jina la akauti ni:- Matombo secondary school self-reliance Namba ya **Akaunti 22101100129** Fedha ilipwe kabla ya kufungua shule. Tafadhli wasiliana na karani wa benki ili aainishe kama ni ada au michango mingine. Risiti ya Benki (pay in slip) utakuja nayo siku ya kufungua shule. Toa photocopy, leta nakala halisi (Original copy) baki na kivuli kwa ajili ya kumbukumbu.

4.0 Mahitaji binafsi ya mwanafunzi anayotakiwa kuleta shuleni:-

Madaftari makubwa ya kutosha kulingana na masomo yake. (Counter books).
Godoro moja la futi 2½.
Blanketi moja (01), Shuka mbili (02) za rangi pink., mto mmoja (01) na foronya mbili (02) pink.
Nguo za ndani za kutosha (chupi, "underskirts"/shimizi, sidiria) na za kulalia (night dress).
Vyombo vya kulia chakula (sahani, kikombe na kijiko)

f) Ndoo ndogo mbili (02).

Kanga au kitenge (jozi moja tu)

Chandarua cheupe kimoja (01).

Taulo, mswaki na dawa ya meno, sabuni na mafuta ya kupaka.

Koti la mvua au mwamvuli.

Vitabu vya ibada kwa mujibu wa dhehebu/dini yako.

Mwanafunzi aje na sanduku la Bati (Tranka), hatupokei masanduku mengine.

m) Shule ina nakala za vitabu kwa ajili ya masomo utakayochukua; hata hivyo kama unaweza kupata vya kwako binafsi uje navyo. (orodha ya vitabu imeambatanishwa uk 10 - 11)

Kama una **Bima ya afya** njoo nayo, kama huna mzazi au mlezi **mkatie binti yako Bima ya Afya.**

Kwa wanafunzi wanaosoma masomo ya Jiografia (Geography) waje na Kikokotoleo (Scientific Calculator) kwa ajili ya kujifunzia darasani.

5.0 Afya ya mwanafunzi:-

Mara upatapo barua hii mwone **Mganga Mkuu wa Hospitali ya Serikali** iliyo karibu nawe, ili upimwe kuthibitisha kuwa una afya ya kutosha kusoma masomo ya sekondari. Fomu maalum imeambatanishwa na barua hii. Mara utakapofika shuleni ioneshe ikiwa imejazwa.

Shule haitoi chakula maalum (special diet) kwa wagonjwa. Hata hivyo ni:-**Ni marufuku kuja na chakula cha aina yoyote hapa shuleni.**

Aidha, kama mtoto ana tatizo la kiafya tafadhali mzazi wasiliana na uongozi wa shule ili tatizo hilo litambulike mapema.

6.0 Sheria za shule:-

Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu na kuwatii wakubwa wote .

Mwanafunzi anapaswa kuwaheshimu wanafunzi wanzake, kuheshimu ukumbi wa mikutano, mahali pa chakula, ofisi za shule, jiko la shule n.k.

Yakupasa kuweka shule, eneo lake na wewe binafsi katika hali ya usafi wakati wote.

Mwanafunzi aheshimu kengele, awahi katika mikusanyiko na kila mahali anapotakiwa.

Mwanafunzi anapaswa kuwa kimya darasani na wakati wa kujisomea.

f) Mwanafunzi anapopata shida kubwa kama kufiwa au kuugua, ruhusa ya kwenda nje ya shule itatolewa na **Mkuu wa Shule** au **Makamu wake.**

Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na simu ya mkononi au viambatanisho vyake kama charger, line, "earphones" pamoja na redio.

Mwanafunzi haruhusiwi **kupiga simu popote** bila kibali cha uongozi wa shule, ili kuepuka upelekaji wa taarifa zisizo sahihi kwa wazazi. Mawasiliano yote yatafanywa kupitia **Ofisi ya mwalimu wa Malezi** tu.

Wanafunzi hawaruhusiwi kuja, au kuletewa chakula cha aina yoyote toka nyumbani.

Mwanafunzi haruhusiwi **kufanya mazungumzo** na ndugu/jamaa yake msikitini, kanisani, au hospitalini. Kama ndugu/jamaa huyo ana maagizo afike ofisini aonane na **uongozi wa shule** .

k) Mwanafunzi haruhusiwi kwenda katika **nyumba za walimu** au **wafanyakazi wengine** bila ruhusa maalum.

Mafuta yenye harufu kali, perfume/spray, poda, rangi za kucha na midomo, wanja, curl, nywele za bandia, mapambo kama bangili, hereni, mikufu n.k**. havitakiwi kabisa shuleni.** Mwanafunzi haruhusiwi kuwa na kucha ndefu wala kujipamba.

Mwanafunzi anatakiwa kuheshimu bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, wimbo wa shule, wimbo wa Tanzania Tanzania Nakupenda kwa Moyo Wote na Tazama Ramani, (Kila mwanafunzi anatakiwa ajue kuimba nyimbo hizi)

Mwanafunzi haruhusiwi kukaa bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi, (Mwanafunzi mgonjwa anapaswa kupumzika katika chumba maalum.

o) Mwanafunzi haruhusiwi kusuka nywele. Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na **nywele fupi wakati wote** wawapo shuleni, urefu **unaowezesha kijiti cha kiberiti kuonekana**. Hairuhusiwi kunyoa kipara au mitindo mingine kama kiduku, kijoti, kiseven n.k.

Mwanafunzi haruhusiwi kubadili dini/dhehebu awapo hapa shuleni.

Ni marufuku **kumruhusu mgeni** kufika katika **eneo la mabwenini**.

Mwanafunzi haruhusiwi kuongea na mtu ambaye si mwanajumuiya wa shule hii isipokuwa **kwa kumsalimia**.

Mzazi/Mlezi aliyeandikishwa shuleni ndiye anaruhusiwa **kumwombea ruhusa mwanafunzi** kama kuna tatizo. Pia ndiye **atakayekuja shuleni** pindi atakapohitajika kufanya hivyo.

Wakati wa kufunga shule wanafunzi wote wataondoka **kwa pamoja kwa usafiri utakaoratibiwa na shule** . Hakuna **ruhusa yoyote itakayotolewa mapema** kabla ya **siku rasmi ya kufunga shule** .

Kama mwanafunzi atapatikana na kosa la nidhamu, mzazi au mlezi ndiye atakayetakiwa kufika shuleni na si mtu mwingine yeyote kama babu, bibi, mjomba,shangazi, kaka n.k.

***7.0 Mwanafunzi atafukuzwa shule au kusimamishwa masomo kwa muda (suspension) iwapo atapatikana na kosa kati ya haya yafuatayo*:-**

Kutukana/kutumia lugha chafu, kumpiga mwalimu au mwanafunzi mwenzake

Kupigana na mwanafunzi mwenzake.

Kuharibu kwa makusudi mali ya umma na ya watu wengine.

Kuolewa.

Kulala nje ya shule bila ruhusa ya uongozi wa shule na utoro wa muda mrefu (miezi 03).

Biashara, ulevi na kutumia dawa za kulevya.

Kuwa na mimba au kuharibu mimba ndani na nje ya shule.

Kuingia na kushiriki kwenye vilabu vya pombe na nyumba za kulala wageni au nyumba zinazouzazo pombe (Guest house au Bar)

i. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu shuleni.

Kukataa kufanya mazoezi na mitihani.

Wizi.

Kudharau bendera ya Taifa.

Makosa ya jinai.

Kunyanyapaa wengine.

Kuleta **simu ya mkononi** au **kukutwa na viambatanishi vyak**e kama charger, betri, vocha, line n.k.

Uasherati, ubakaji, ushoga na ulawiti.

Kukaa au kulala bwenini wakati wa vipindi au wakati wa kazi nje.

Kama unakubaliana na **haya yote** yaliyoelekezwa na **uko tayari kuyatii** na **kuyatekeleza**; tia saini katika fomu iliyoambatanishwa. Fomu hii ya kujiunga na shule inatakiwa **irudishwe ofisini** pamoja na **fomu ya kupimwa iliyojazwa na mganga** wa hospitali **ya serikali**.

Nakutakia safari njema.

KARIBU SANA

.....

MARIAM R. MADAMBA

MKUU WA SHULE

AHADI YA MWANAFUNZI

Mimi.....

Nimesoma na kuelewa yote yaliyoelekezwa kwenye barua ya kujiunga na shule.

Ninaahidi kuwa nitajifunza kwa bidii zangu zote, nitazingatia sheria za shule kama zilivyoainishwa, nitazifuata na nitakuwa na nidhamu wakati wote kwa manufaa yangu, ya shule na ya taifa kwa jumla.

…… …….. ……

Saini ya Mzazi/Mlezi **Tarehe** **Saini ya Mwanafunzi**

MATOMBO SECONDARY SCHOOL,
P.O.Box749,
MOROGORO.

DATE .....

Ref. No.....

PART A:-
To the Medical Officer,
.....
.....
.....

REF: .....
Please examine the above named student as to her physical and mental fitness for being student. Each defect will hinder a girl for Secondary Schools' education.

1. a). Eye sight
   b). Hearing
   c). Limbs
   d). Speech
   e). Venereal disease
   f). Leprosy
   g). Epilepsy

Neurosis
Other serious diseases
Pregnancy

PART B: MEDICAL CERTIFICATE

(To be completed by a **GOVERNMENT MEDICAL OFFICER**)

I have examined the above named student and confirm that she is physically fit/not fit for a full time Secondary School Education.

a). Eye sight .....
b). Hearing .....
c). Limbs .....
d). Speech .....
e). Venereal diseases .....
f). Leprosy.....
g). Epilepsy.....
h). Neurosis.....
i). Other serious diseases.....
j). Pregnancy.....

Name..... Signature..... Date.....

STATION..... **DESINATION**.....
N.B . I request this form to be returned to the school in a sealed envelope.

FOMU YA HISTORIA YA MWANAFUNZI

JINA LA MWANAFUNZI.....

JINA LA MZAZI/MLEZI WA MWANAFUNZI.....

JINA LA SHULE ANAKOTOKA.....

TAREHE YA KUZALIWA.....

KATA ANAYOTOKA MWANAFUNZI.....

WILAYA ANAYOTOKA MWANAFUNZI.....

MKOA ANAOTOKA MWANAFUNZI.....

KABILA.....

URAIA.....

DINI/DHEHEBU.....

ANUANI YA MZAZI/MLEZI.....

NAMBA YA SIMU YA MZAZI/MLEZI - NYUMBANI.....

OFISINI.....

E - MAIL ADRESS.....

ANUANI YA POSTA KWA AJILI YA KUTUMA MATOKEO YA MITIHANI: -

.....

.....

MAJINA MANNE YA NDUGU WA KARIBU WALIOIDHINISHWA KUCHUKUA NAFASI YA MZAZI/MLEZI ENDAPO DHARURA ITATOKEA:-

Na	**JINA**	**UHUSIANO**	**ANAKOISHI**	**NAMBA YA SIMU**
01.				
02.				
03.				
04.				

MATOMBOSECONDARY
SCHOOL A-LEVEL BOOKS
REQUIREMENT

GEOGRAPH PAPER I

Principles of Physical Geography- by F.J Monkhouse
A comprehensive Approach to Physical Geography for Secondary School- b y D.T Msabila
Practical Geography for Africa by John M. Prichard
Land forms in Africa – An introduction to Geomorphology – by Colin Buckle
Africa – by J.M. Prichard
Practical Geography for A level – by Francis Mnyawi

GEOGRAPH PAPER II

Human and Economic Geography – by Goh cheng & Morgan
Advanced Level geography Course book –by Tanzania Institute of Education (TIE)
An Integrated Focal regional study on Human and Economic Geography Advanced level paper 2- by D.T Msabila

ENGLISH LANGUAGE
NOVELS AND SHORT STORIES

Chinua Achebe – A man of the people
Ayi Ewei Armah – The Beautiful ones are not yet born
Soga – His Excellence the head of state.

PLAYS

I wi l marry when I want by Ngugi wa Thiong'o & Ngugi wa Mir i
An Enemy of the people by H. Ibsen
The Caucasian Chalk Circle by B. Bretch
Betray in the city by F. Imbuga

POETRY

Tanzania Institute of Education – Selected poems
David Cook et al – Poems from East Africa

NB: Make sure you come with TWO tiltles from each part.
This list of English Language is meant for HGL students only.

HISTORY

Rodney, W – How European Underdeveloped Africa
Nyirenda, H.D – Africa in World History – A level Notes
Nabudere, D.W – Essay on the Theory and Practices of Imperialism
Lenin V.I. Imperialism the highest stage of capitalism
Nyangwine, N. advanced Level – History Notes, Selected topics for paper 1&2
World Map, Africa Map, East Africa Map and Tanzania Map.

KISAHILI: I

Historia ya matumizi ya Kiswahili, Mbunda
Msokile (1992), Education Publishers and Distributors Ltd
Kiswahili sekondari. Taasisi ya Ukaguzi Mitaala (1958)
Sarufi ya Kiswahili Sekondari na na Vyuo James S. Mdee (1988), DUP
Kiswahili kidato cha Tano. TIE

KISWAHILI: II

Fasihi . Senkoro F.E.M.K. (2011) Kauttu Limefed DSM) (2011)
Kamusi ya Kiswahili Sanifu (TUKI – DSM) Toleo la pili

RIWAYA

Kufikirika Shaaban Robert T. Mkuki na Nyota
Publishers Dar es Salaam, (2003)
Mfadhili, Hussen Tuwa Macmillan AIDAN (2007)
(iii)Usiku utakapokwisha – Mbunda Msokile, Macmillan.

USHAIRI

Mapenzi bora Shaaban Robert, Mkuki na Nyota Publishers (2007).
Chungu Tamu T.A. Mvungi, TPH Dar es salaam (2004).
Fungate ya Uhuru, Muhamed Seif Khatibu, DUP, Dar es Salaam, (2000).
Kimbunga, Haji GORA HAJI tuki Dar es salaam, (2003).

Note: Knowledge is acquired through Books but Skills is Obtained by Practice.

Bring with you at least two books from list above

KIAMBATISHO: SARE ZA SHULE NA GHARAMA ZAKE

Uniform zinapatikana shuleni kwa bei zifuatazo:

Skirt blue (moja) -25000/=Shati jeupe (moja)
12000/= T-shirt blue bahari (moja) -12000/=
sweater (moja) 15000/=Hijabu white & blue (moja) 15000/=
skirt shamba (moja) 20000/=Nembo 10000/=

(Mwanafunzi anashauriwa kuwa na pea mbili kwa uniform zote zilizoorodheshwa hapo juu)

Track suit ya michezo Tsh 30000

Sare zote zinapatikana shuleni zikiwa na nembo ya shule mwanafunzi aje na pesa mkononi, zisiwekwe kwenye akaunti.